

maji kutoka kisimani kwa kutumia simu ya mkononi...  
Lymo (kulia) mbunifu wa mfumo huo. Maonyesho ya 17 ya Elimu ya Juu Sayansi na Teknolojia ya Mwananchi ya Mlazi  
Mmoja, Dar es Salaam juzi. (Picha na Yusuf Badi).

HABARI LEO UK 8.

# \* Watanzania wahimizwa kula nyama zaidi \*

Na Anastazia Anyimike

**I**MEELEZWA kuwa pamoja na ongezeko la uzalishaji wa kuku, ulaji wa nyama kwa mtu mmoja kwa mwaka bado ni mdogo kitaifa ambapo takwimu zinaonesha ni kilo 15 kati ya 50 zinazopendekezwa na Shirika la Chakula Duniani (FAO).

Aidha, imeelezwa kiwango cha sasa cha ulaji wa mayai kwa mtu mmoja kwa mwaka ni 106 wakati mapendekezo ya FAO kiasi kinachotakiwa ni 300.

Hayo yalibainishwa juzi jijini Dodoma na Nibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega wakati wa kikao cha Wizara na wadau wa tasnia ya kuku na alisema juhudi zinahitajika kuendelea kuhamasisha wananchi kutumia nyama ya kuku ili kufikia kiwango kinachoshauriwa na FAO.

Ulega alisema takwimu za mwaka 2021/2022, Tanzania ina kuku milioni 92.8 ambapo kuku wa asili ni milioni 42.7 na kuku wa kisasa ni milioni

50.1.

Alisema kaya zinazojishughulisha na kilimo na ufugaji ni zaidi ya kaya milioni 7, kati ya hizo kaya zaidi ya milioni 4 sawa na 55.3 wanafuga kuku, hii inaonesha ufugaji wa kuku ni muhimu kwa uchumi wa wananchi wengi nchini.

"Ulaji wa nyama kwa sasa ni kilo 15 kwa mtu kwa mwaka, aidha kati ya hizo ni kilo 2 tu zinatokana na nyama ya kuku, hali kadhalika ulaji wa mayai kwa sasa ni 106 kwa mtu kwa mwaka takwimu ambazo zipo chini," alisema Ulega.

Alisema sekta ya kuku imekua kwa kasi miaka ya hivi karibuni kutokana na kuwepo kwa soko linalotokana na ongezeko la watu na kipato, uwekezaji na uwepo wa mazingira bora katika tasnia ya hiyo.

Ulega alitaja sababu nyingine ni kuwepo urahisi wa kufuga kuku na uwezekano mkubwa wa kuwamiliki kuliko wanyama wakubwa, uwepo wa Taasisi mbalimbali zinazotoa mikopo kwa vijana na akina mama na vikundi mbalimbali am-

bao wengi wamejizatiti katika biashara ya kuku.

Alisema kuwepo kwa faida zote hizo na soko kubwa la kuku hapa nchini, suala la upatikanaji wa vifaranga na vyakula vya kuku limekuwa likipanda na kushuka katika msimu wa mwaka.

"Katika kipindi cha mwaka 2019 ulipozuka ugonjwa wa Corona ilileta athari kubwa katika mnyororo wa thamani wa tasnia ya kuku. Pamoja na changamoto hizi nina imani katika kikao hiki tutajadili kwa mapana yake namna ambavyo sekta mbalimbali zitashiriki kwenye utatuzi wa changamoto zilizopo katika tasnia hii," alisema.

Ulega alitumia nafasi hiyo kuwashukuru wadau mbalimbali wakiwemo taasisi za kifedha na wadau wa maendeleo kwa michango yao katika Sekta ya mifugo.

Aidha, alitoa rai kwa taasisi za kifedha kuona namna ya kuwekeza katika mnyororo wa thamani ili kuchagiza ya ustawi wa tasnia ya kuku, kupitia ushirikiano wa Serikali na Sekta binafsi (PPP).



MAKAO M

HABARI LEO UK 5

## \* Wafugaji waunganishwa kutumia fursa za kifedha \*

**J**UMLA ya vikundi 400 vya wafugaji mkoani hapa vimeunganishwa na kusajiliwa kwa malengo ya kuweza kutumia fursa zilizopo za mikopo nafuu kutoka taasisi za kifedha.

Kauli hiyo imetolewa na Mkuugenzi Mkuu wa Dodoma Halisi Limited, Anthony Msanga wakati akizungumza katika kikao cha wadau wa maziwa.

Kikao hicho pia kilitumika kufanya uzinduzi wa kampeni ya ufugaji ng'ombe wa kisasa wa maziwa kilichofanyika katika Wilaya ya Chamwino.

Alisema kuwa kampuni hiyo imeweza kuwaweka katika umoja vikundi hivyo kwa lengo la kuwaunganisha pamoja ili waweze kupata fursa ya mikopo ikiwa kuwaelimisha elimu ya ufugaji bora wa ng'ombe wa maziwa kwa ufanisi zaidi.

"Elimu hiyo ya ufugaji bora wa ng'ombe wa maziwa ikiwemo na kitendo cha kuwaunganisha kwa pamoja ni imani yetu wataweza sasa kupata fursa za mikopo nafuu kwa urahisi na hatimaye lengo letu la kuamsha ufugaji bora wenye tija kibiashara watafanikiwa kutimiza ndoto zao" alisema.

Alisema kuwa kampuni hiyo imejipanga kuhakikisha inakuwa na ng'ombe wa kisasa wa mbegu bora, malisho chakula maji pamoja na elimu ya kuaandaa na kuhifadhi malisho ya mifugo.

Aidha itahakikisha uwepo wa mabanda bora ya ng'ombe na elimu ya ufugaji wa kibiashara pamoja na upatikanaji wa chanjo sahihi, virutubisho na matibabu ya uhakika kwa ng'ombe ili mfugaji aweze kupata faida.

Mkuu wa Wilaya ya Chamwino Gift Msuya amewataka wananchi kunywa maziwa kwa wingi ili waweze kuimarisha afya zao ambayo yaliyo safi na salama yaliyopimwa na kuchemshwa kwa viwango.

Pia amewataka wafugaji kuhakikisha wanatumia fursa ya ufugaji kwa kuungana kwa pamoja ili waweze kuunda vikundi ambavyo vitakavyowawezesha kupatiwa mikopo kwa ajili ya uboreshaji na ufugaji wenye tija.

"Niwasilhi wafugaji ni wakati sasa wa kuachana na ufugaji wa kizamani, tumieni fursa ya kufuga mifugo michache ili waweze kupata faida atakayoweza kuwamudu katika kuwahudumia" alisema.

Aidha alizitaka pia taasisi na makampuni mengine kutoa fursa ambazo zinazowagusa jamii katika kujipatia mahitaji maalumu kama ilivyo kwa kampuni ya Dodoma Halisi ambayo imeweza kuwaunganisha wafugaji 400 kwa ajili ya kujipatia mikopo.

W

W

M

funzi v  
mafun  
kuhak  
ifu na

Ali

elimu

kazi w

na she

sheria

yake r

kuend

Ali

wakat

kikao

kutok

Dodo

inaoitana kwa masilahi zote hali ambayo inatathmini  
usalama wa miamala.

baada ya Rais Samia Suluhu Hassan  
san kukagua gwaride shughuli itakuwa  
imekwisha na wananchi wataondoka

Mzumbe Morogoro, Mariki Malupu  
aliomba serikali itoe elimu ya kutosha

tujiulize tutalifanyia nini Taifa letu "  
alisema Ibangi.

HABARI LEO UK 3.

# \*Dk Mpango aonya wanaopokea fedha kulinda wafugaji\*

Na Swaum Katambo, Katavi

**M**AKAMU wa Rais, Dk Philip Mpango amewaonya viongozi wa serikali na Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Katavi wanaopokea fedha ili kuwalinda wafugaji wanaopeleka mifugo kwenye maeneo ya hifadhi.

Alitoa onyo hilo wakati akizungumza na wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika mkoani humo alipokwenda kukabidhi hundi ya shilingi Bilioni 2.3 kwa viongozi wa vijiji 8 vilivyo katika mradi wa kuvuna hewa ya ukaa pamoja na kuzindua mradi wa maji Sibwesa.

"Ninafahamu, mimi ndio msaidizi mkuu wa mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, lakini pia nina kofia nyingine mimi ni mjumbe wa kamati kuu ya Chama Cha Mapinduzi

kwa hiyo ninawaasa viongozi wa Serikali na Chama, viongozi lazima tuongoze kwa mfano hatuwezi kuwa sisi wenyewe ndio sehemu ya tatizo" alisema Dk Mpango na kuongeza;

"Tunapokea fedha halafu tunawalinda wanaopeleka mifugo kwenye maeneo ya hifadhi; hili ninawaomba ninawataka muache, narudia tena hili muache."

Dk Mpango alionya wakulima na wafugaji wanaohama mara kwa mara kuacha tabia ya kuwapatia fedha viongozi.

"Lakini pia hicho kilimo cha kuhamahama watu wanaenda huko kwenye hifadhi lakini kwa sababu wanawapatia fedha baadhi ya viongozi, viongozi wa namna hii wajipime, na tutawawekea jicho kali zaidi" alisema.

Dk Mpango alizindua mradi wa maji wa Sibwesa uliopo Wilaya ya Tanganyika mradi uliogharamu Sh milioni 173.2 ukiwanufaisha wananchi zaidi ya elfu saba wa Kijiji cha

Sibwesa.

Mradi huo ni kati ya miradi ya maji ili iotekelezwa kwa kutumia fedha za ustawi wa taifa na mapambano dhidi ya Covid-19.

Akizungumza na wananchi wa Wilaya ya Tanganyika mara baada ya kuzindua mradi huo, Dk Mpango alisema serikali itaendelea kutekeleza miradi ya huduma za kijamii kama vile maji, elimu na afya ili kuwasaidia wananchi kufikia maendeleo ya haraka.

Mradi huo umewezesha kupatikana kwa maji safi na salama katika taasisi zote zilizopo eneo la sibwesa pamoja na kuwasaidia wananchi kuondokana na maradhi yatokanayo na maji yasio safi yalikuwa yakipatikana hapo awali.

Akiwa katika Kijiji cha Sibwesa Dk Mpango aliagiza kupelekwa kwa mtaalamu wa kilimo katika Kijiji hicho ili kuweza kuwasaidia wananchi kufanya kilimo cha kisasa na

kuongeza uwingi wa upatikanaji wa mazao.

Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi alisema sera ya wizara ya maji ni kuhakikisha huduma ya maji inafikishwa katika taasisi zote za kiserikali na zisizo za kiserikali.

Alisema pamoja na uwepo wa mradi huo serikali inatarajia kutekeleza mradi wa shilingi bilioni 1.8 ili kusaidia wilaya hiyo katika vijiji vine vya vya Nkungwi, Kasekese, kaseganyama na Sibwese.

Mwakilishi wa wananchi ambaye ni mbunge wa Mpanda vijijini Selemani Kakoso aliipongeza serikali kwa kutekeleza mradi huo.

Akiwa katika Kijiji cha Centre Maria, Makamu wa Rais ameigiza wizara ya Nisnati kuhakikisha inatatua changamoto ya kukatika kwa umeme katika eneo hilo na Katavi kwa ujumla.

## HABARI DODOMA

NIPASHE UK 15

### \* Vikundi 400 vya-unganishwa kupata mikopo

Na Peter Mkwavila,

CHAMWINO

VIKUNDI 400 vya wafugaji na wakulima katika wilaya za Kongwa na Mpwapwa mkoani Dodoma, vimeunganishwa na kusajiliwa ili kupata mikopo nafuu kwa taasisi za fedha.

Mkurugenzi Mkuu wa Dodoma Halisi Limited Tanzania, Anthony Msanga, aliyasema hayo jana katika kikao cha wadau wa maziwa sambamba na uzinduzi wa kampeni ya ufugaji ng'ombe wa kisasa wa maziwa wilayani Chamwino.

Alisema kampuni hiyo imefanikisha kuunganisha ili kupata fursa ya mikopo na elimu ya ufugaji bora wa ng'ombe wa maziwa.

"Elimu hiyo ya ufugaji bora ya ng'ombe wa maziwa ikiwamo na kitendo cha kuunganisha kwa pamoja, ni imani yetu wataweza sasa kupata fursa ya mikopo nafuu kwa urahisi na hatimaye lengo letu la kuamsha ufugaji bora wenye tija kibashara watafanikiwa kutimiza ndoto zao," alisema.

Hata hivyo, alisema kampuni imejipanga kuhakikisha wafugaji wanafuga kisasa na kuwa na uhakika wa malisho na maji.

Alisema elimu inayotolewa ni pamoja na namna ya kuanadua na kuhifadhi malisho ya mifugo.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Chamwino, Gift Msuya, aliwataka wafugaji kuhakikisha wanatumia fursa ya ufugaji bora na wenye tija kupitia vikundi hivyo.

"Niwasili wafugaji ni wakati sasa wa kuachana na ufugaji wa kizamani, tumieni fursa ya kufuga mifugo michache ili kupata faida atakayoweza kuwamudu katika kuwahudumia," alisema.

Aidha, alizitaka pia taasisi na kampuni zingine kutoa fursa ambazo zinazowagusa jamii na zinazowainua kiuchumi.



Mkurugenzi Mkuu wa Dodoma Halisi Limited, Anthony Msanga, akizungumza na wadau wa maziwa wa Mkoa wa Dodoma kwenye uzinduzi wa kampeni ya ufugaji ng'ombe wa maziwa wa kisasa uliofanyika Chamwino jana. wengine waliokaa (wa tatu kushoto) Mwenyekiti wa Maaridhiano Mkoa wa Dodoma, Askofu Evance Chande na (wa pili kulia) Mkuu wa Wilaya ya Chamwino, Gift Msuya. **PICHA: PETER MKWAVILA**

## RC atoa siku 10 h'shauri kupitia taarifa za usambazaji dawa

Na Paul Mabeja, DODOMA

**M**KUU wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mataka, ametoa siku 10 kwa waturugenzi wa halmashauri za mkoa huo kukutana na kupitia taarifa za upokeaji, utoaji na usambazaji wa dawa kwenye mae-neo yao.

Vile vile, amewataka kuchukua hatua za kinidhamu kwa watumishi ambao watabainika kuhusika na upotevu au upungufu wa dawa katika zahanati, vituo vya afya, hospitali za wilaya na mkoa.

Mtaka alibainisha hayo jijini hapo katika kikao chake na viongozi wa wilaya katika sekta ya afya, kwa ajili ya kupitia taarifa ya upokeaji, utoaji na usambazaji wa dawa.

"Hizi siku 10 tunazopeana ziwe za kazi ambazo lengo lake ni kufanya ukaguzi na kujiridhisha kwa dhiti kuhusu matokeo ya dawa kwenye vituo vya afya, zahanati, hospitali za wilaya na mkoa. Baada ya hapo kutakuwa na kikao cha kupokea taarifa na kutapobainika upungufu waturugenzi wanayo nafasi ya kuchukua hatua za kinidhamu."

"Tutakaa kikao kingine cha kupokea taarifa ya ukaguzi wa vi-

tuo vya afya, zahanati, hospitali za wilaya na mkoa kwa asilimia 100 katika upokeaji, utoaji na usambazaji wa dawa na baada ya hapo katibu tawala wa mkoa ataweza kuchukua hatua kwenye maeneo ambayo yameonyesha upungufu," alisema.

Kadhalika, alisema taarifa itakayotolewa na waturugenzi ionyeshe dawa kiasi gani zimepokelewa, thamani ya dawa, thamani ya upungufu na upotevu ili kulinganisha waliyopokea kutoka serikali kuu na wadau wengine.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kongwa, Dk. Omary Nkullo, alisema kikao hi-

cho ni muhimu kutokana na serikali kutoa fedha nyingi kwa ajili ya kuboresha huduma za afya.

Alisema maelekezo yaliyotolewa na Mkuu wa Mkoa wameyachukua na wanaenda kuyafanya kazi na kuhakikisha siku 10 alizotoa wanapitia taarifa na kuchukua hatua kama walivyogizwa.

"Kikao kimeenda vizuri na sisi tukiwa kama wasimamizi wakuu wa fedha katika ngazi ya wilaya tutahakikisha tunapitia taarifa kama tulivyoagizwa na pale ambapo tut-aona kuna haja ya kuchukua hatua hatutasita kufanya hivyo," alisisitiza Dk. Nkullo.

## \* Watakiwa kujiepusha rushwa uvalishaji hereni mifugo

Na Renatha Msungu, DODOMA

MKUU wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri, amewataka wataalamu wa mifugo kupeuka kuomba rushwa kwa wafugaji katika uvalishwaji hereni mifugo.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa zoezi hilo katika Kata ya Nata jijini hapo

mwishoni mwa wiki, Shekimweri alionya wataalamu hao kuhusu malalamiko ya kuomba rushwa kutoka kwa wafugaji.

"Naomba mkafanye zoezi hili kwa uaminifu nahitaji kusikia idadi ya mifugo ili-yopangwa kuvishwa hereni katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma inafikiwa yote," alisema Shekimweri.

Aidha, aliwataka wataalamu kutumia lugha nzuri kwa wafugaji na kuwatumia viongozi wa kimila ili kufanikisha zoezi hilo.

Mkuu huyo alisema endapo zoezi hilo litafanikiwa kwa kiwango kikubwa migogoro baina ya wafugaji na wahifadhi ya kulalamikia kubambikiziwa kesi ya kuingiza mifugo itakwisha.

"Ni vyema suala hilo mkalikamilishe kwa sababu itasaidia serikali kujua nani kaingiza mifugo kutokana na mifugo itakuwa na hereni, lakini kuwatetea wafugaji endapo hawatafanya kosa hilo ili wahifadhi watadai wamefanya," alisema Shekimweri.

Naye ofisa mifugo wa jiji hilo, Gratian Msigwa, alisema wanatarajia kuvishwa he-

reni mifugo 50,000 na Sh. milioni 33 zitatumika katika zoezi hilo.

Alisema ni lazima mifugo yote ichanjwe na kuongeza kuwa atakayekaidi suala hilo hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

Aliwahimiza wafugaji kutoa ushirikiano kwa wataalamu wanapoendesha zoezi hilo bila kikwazo.

# Prof Muhongo: Why cage fish farming is crucial

By DAILY NEWS  
Reporter

CAGE fish farming is increasingly becoming crucial as fishermen experience a declining stock of fishes in Lake Victoria, says Musoma Rural Member of Parliament, Prof Sospeter Muhongo.

"There is a significant decrease in the number of species of fish in Lake Victoria, the solution now is cage fish farming," said Prof Muhongo.

And looking to promote the fishery sector and improve fish production, Musoma DC has embarked on promoting cage fish farming.

Prof Muhongo said the Musoma DC has been making deliberate efforts to improve fisheries, one of the key economic activities for people along Lake Victoria.

According to the former Energy and Minerals Minister, fishermen in Musoma constituency have been forming fishery cooperatives and groups in order to secure fishing tools through loans or sponsors.

Musoma DC has registered five fishery cooperatives so far, namely; Kome Fisheries Cooperative Ltd, Kasoma Fisheries Cooperative Ltd, Bwaikumsoma Fish-

eries Cooperative Ltd, Busumi Fisheries Cooperative Ltd and Kurukiri Fisheries Cooperative Ltd.

According to Prof Muhongo at least five fishery groups, including Kurwera from Busamba Village, were finalising their registrations.

Others are from four islets of Rukuba, Kagongo, Muloba and Nyasaungu.

Cage farming involves keeping fish in any type of enclosure and holding them captive within an enclosed space whilst maintaining a free flow of water.

The cage culture is receiving more attention by both researchers and commercial

producers due to factors such as increasing consumption of fish, declining stocks of wild fishes and poor farm economy.

In the 2022/2023 budget, the government unveiled plans to introduce cage fish farming to grow the economy and increase the sectors contribution to the GDP.

Tanzania has total inland water surface area covering 62,000 square kilometers, comprising the four main water basins of: Lake Victoria, Nyasa, Tanganyika and Rukwa.

The country also encompasses a territorial sea size of 64,500 square kilometers.

These resources offer investment opportunities in fishing, fish farming and salt harvesting. Despite this enormous potential, statistics indicate that fishing and aquaculture account for 2.2 per cent of the national gross domestic product (GDP), 3 per cent of foreign earnings, engage some 200,000 and 4.2 million people in permanent and temporary employment respectively.

If well utilized, the fishery sector can be the engine of economic growth, source of food and employment, the basis of socio-economic development and industrialisation.

## DODOMA NEWS

ALL Stories from BEN BAGO in Dodoma

# Over 100,000 livestock to have tag earrings

THE DODOMA City Council plans to track, identify, and register over 100,000 livestock by placing on them electronic tag earrings with the aim of controlling diseases and livestock theft.

The plan was revealed recently by the Dodoma City

Council Head of the Livestock and Fisheries Department, Gratian Mwesiga, when presenting report to Dodoma District Commissioner on the identification, registration and monitoring of livestock and the exercise of putting electronic earrings to the livestock during

the launch of the exercise held in Nala area in Dodoma.

Mwesiga said the Dodoma City Council expects to identify and put on cattle tag earrings to about 50,000 cows, 45,000 goats, 10,000 sheep and 200 donkeys.

Speaking about the imple-

mentation of the exercise, he said that the Dodoma City Council set aside 33m/- for the implementation of the exercise.

"The government issued a guideline for running the exercise of putting on tag earrings. Among others, the guideline

directs the price of earrings not to exceed 1,750/- for cows and donkeys, while 1,000/- for goat and sheep," he noted.

Expressing the importance of the exercise, Mr Mwesiga said the identification, registration and monitoring of livestock have many benefits.

"Livestock will be recognised and can be traced wherever they are and who owns them. The system also helps to control diseases including epidemics," he added.

He also noted that the move ensures food safety and facilitates the trade of livestock

and its products inside and outside the respective area as well as controlling livestock theft.

Mr Mwesiga added that the exercise will facilitate and enable herders to have access to loans and livestock insurance.

On his part, Mr Elisha

Msangi, who is a breeder, said the exercise of identification, registration and monitoring of livestock will ensure the safety of their livestock.

"We believe that this exercise will put an end to livestock theft experienced by livestock herders," he said.

## Dodoma outlines measures for effective supply of medicines

DODOMA region has put in place strong measures for ensuring good and effective delivery and distribution of medicines in all district health facilities.

To make the plan successful, Regional Commissioner Anthon Mtaka has given 10-day ultimatum to the directors of all councils in the region to meet and review report on the receipt, delivery and distribution of medicines in their districts.

RC Mtaka issued the directives recently during his meeting with the district leaders in the health sector and council directors, a meeting was aimed at resolving challenges in the delivery and distribution of medicines and medical equipment in the region.

Mr Mtaka also asked the directors to institute disciplinary measures against employees causing loss or shortage of medicines in clinics, health centres, and district and regional hospitals.

"These 10 days that we are giving should be used for carrying out groundwork to conduct an inspection to satisfy ourselves sincerely about the status of availability of medicines at health centres, clinics, district and regional

hospitals," he said.

"After that, there will be a meeting to receive report and where deficiencies are identified, the directors have the opportunity to take disciplinary measures to your subordinates who are found guilty of creating problems," he added.

According to the RC, there will be another session to receive a report on the inspection of health centres, clinics, district and regional hospitals on the distribution and delivery of drugs after which regional administrative secretaries will be able to take actions in areas that will have shown shortfalls.

He said that the report that will be submitted by the directors should show the amount and value of medicine received so that a comparison can be made to establish the medicine allocated and the consignment delivered.

For his part, Kongwa Executive District Director Dr Omari Mkulo commended the move, admitting that the "government has been channeling a lot of money to improve health services."

He said the directives of the regional commissioner will be implemented.



AN excavator proceeds with the preparatory work for the expansion of Nyerere Road near Chang'ombe flyover in Dar es Salaam as captured yesterday. (Photo by Mohamed Mamba)

## War veterans welcome decision to restore Heroes Day celebrations

THE Veterans of the Second World War (World War II) have applauded the government for reinstating the Heroes Day celebrations.

The day is usually marked on every 25 July to honour all soldiers who fought for the country in different wars but the day has not been celebrated for past five consecutive years.

Speaking to reporters at the Mashujaa grounds in Dodoma during the final preparations for the celebrations, General Secretary of the Association

of Retired Soldiers who fought in the Second World War, Charles Lubala said war veterans are happy with the government decision to restore the celebrations because it is necessary to remember the past.

Mr Lubala thanked President Samia for re-introducing the celebrations as it is a great pride for them as heroes who fought for the nation, he noted.

According to Lubala, by restoring the celebrations President Samia has

shown appreciation for their efforts they made in fighting for the nation.

"Actually, we as an association of retired soldiers who fought in the second World War ( World War II) are very relieved to see President Samia bringing back this day that will be celebrated in every region," said Lubala.

On his part, veteran Omary Shanzazi (103), who participated in the Second World War, explained how he participated in the war until he returned home safely while having lost many of

his friends, some of whom were killed by a bomb on a ship by Nazi tyrant Adolf Hitler when they were on their way to military missions.

"I have lost many of my friends, some of them were shot down in the ship while sailing to Egypt on the military mission, and others drowned" recalled Mzee Omary.

He asked the government to honour them and give them their respect as they are the ones who fought for this nation.

National Heroes Day celebrations for 2022 are being held today in Dodoma where President Samia, who is Command In Chief of Armed Forces, is expected to be the chief guest.

Prime Minister Kassim Majaliwa ordered every region to commemorate the day.

Speaking to the press after inspecting the preparations at the Mashujaa grounds in Dodoma City, the premier expressed his satisfaction with progress.